JARILA LA ROBO YA KWANZA (JULAI - SEPTEMBA) 2023/2024

# MAKAMBAKO YETU

www.makambakotc.go.tz | Kitengo cha Mawasiliano Serikalini | Halmashauri ya Mji Makambako



## BAADA YA WAFANYABIASHARA WA SOKO LA NYANYA KUSUASUA KUJENGA VIBANDA,BARAZA LA MADIWANI LAAZIMIA MWANANCHI YEYOTE MWENYE UWEZO WA KUJENGA APEWE MKATABA WA UJENZI

>>> Kila mwananchi ruksa kujenga kwa kufuata utaratibu uliowekwa kulingana na mkataba wa ujenzi >>> Kuhusu matumizi ya dampo la Itengelo baraza lasema halifanyii kazi vyombo vya habari... soma uk. 1&2



**BAADA YA WAFANYABIASHARA WA SOKO LA NYANYA KUSUASUA KUJENGA VIBANDA,BARAZA LA MADIWANI LAAZIMIA MWANANCHI YEYOTE MWENYE UWEZO WA KUJENGA APEWE MKATABA WA UJENZI.**

## Kila mwananchi ruksa kujenga vibanda soko la nyanya.

**Na. Lina Sanga**

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Makambako limeazimia ujenzi wa soko la nyanya katika Kata ya Mjimwema kuruhusu wananchi wote wenye nia ya kujenga vibanda katika soko hilo,kwani wadau waliokuwa wakifanya biashara katika soko hilo wameonyesha kushindwa kukamilisha ujenzi ndani ya muda uliopangwa na wengine kutojitokeza kabisa.

Azimio hilo lilitolewa novemba 7,mwaka huu katika mkutano wa baraza la Madiwani katika kipindi cha kuishia robo ya kwanza (julai – septemba)katika mwaka wa fedha 2023/2024 mara baada ya diwani wa Kata ya Mjimwema,Mhe. Nolasko Mlowe kuhoji hatima ya ujenzi wa soko hilo kutokana na ujenzi kusimama kwa muda mrefu.

Mhe. Hanana Mfikwa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako ambaye ndiye Mwenyekiti wa baraza la Mdiwani alisema kuwa,suala la ujenzi wa soko la nyanya limechukua muda mrefu ,hivyo kwa sasa ni wakati wa kila mwananchi kutangaziwa kuhusu fursa ya ujenzi wa vibanda katika soko hilo kwani wadau ambao walikuwa wakifanya biashara katika soko hilo wameonyesha wazi  kuwa hawawezi kujenga.



**Pichani: Ni jengo la  vibanda 20 vilivyoanza kujengwa  katika soko la nyanya,kwa mfumo wa jenga,tumia,rejesha.**

Alitoa wito kwa wananchi wote wenye nia ya kujenga vibanda kwenye soko hilo ndani ya muda uliopangwa,kufika katika ofisi ya Mkurugenzi ili wapewe utaratibu na kusaini mkataba wa ujenzi ili Halmashauri ipate mapato na wananchi wapate huduma.



“Mheshimiwa diwani wa eneo husika kawaelimishe watu  wako kwamba sisi Halmashauri  tumengojea kwa muda wa kutosha, mtu yeyote ambaye hata kuwa na uwezo au nia ya kujenga,sisi tunampatia mtu mwingine tusiwe na lawama yoyote,zaidi ya miaka mitano tunaongea kitu kama hicho ni watu wa ajabu hatuwezi tukafika kwa namna hiyo ,lazima kitu chochote kiwe na mpaka wa muda ,hivyo yeyote anayetaka kujenga vibanda afike kwa Mkurugenzi apewe mkataba na apewe eneo ajenge vibanda ndani ya muda unaotakiwa na hakutakuwa na nyongeza za hovyo hovyo katika mikataba ya namna hiyo,habari ya tumenyang’anywa vibanda wamepewa matajiri tumewatangazia na tumevumilia kwa muda mrefu,vibanda anajenga mtu yeyote bila kuathiri mikataba”,alisema Mhe. Hanana.



**Pichani: Ni vibanda vya zamani katika soko la nyanya,ambalo linatakiwa kujengwa upya kwa mfumo wa jenga,tumia,rejesha.**

Awali akijibu hoja hiyo, Bi. Appia Mayemba,Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako amesema kuwa,zoezi la ujenzi wa soko la nyanya lilitangazwa ,kipaumbele ilikuwa wadau waliokuwa wanafanya biashara katika soko hilo na walipatikana  wadau ishirini na kuna ujenzi wa vibanda 20 utaendelea baada ya kuongezewa mkataba mpya na kwa sasa kila mwananchi anaruhusiwa kujenga kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwani wadau waliokuwa sokoni hapo hawaonyeshi ushirikiano.



**Baraza la Madiwani laishauri Menejimenti kuhusu uwekezaji.**

**Na. Lina Sanga**

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Makambako limeishauri Menejimenti kuendesha miradi ya uwekezaji kwa faida ili kuanzisha miradi mipya ya uwekezaji na kuongeza mapato ,badala ya kukopa kwa ajili ya kuanzisha miradi mipya ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mzani katika soko la mazao lililopo Mtaa wa Makatani,Kata ya Lyamkena.

Ushauri huo ulitolewa novemba 7,mwaka huu katika mkutano wa baraza la Madiwani katika kipindi cha kuishia robo ya kwanza (julai – septemba) katika mwaka wa fedha 2023/2024,uliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri.

Wakitoa ushauri huo kwa nyakati tofauti wajumbe wa baraza hilo walisema kuwa, ombi la kukopa fedha kwa ajili  kuingizwa kwenye biashara ya mzani ambao Halmashauri haijawai kuifanya halikubaliki,hivyo ni vema mradi huo ubinafsishwe au kujengwa  kwa mfumo wa jenga,tumia,  reje-

sha ili kutoa fursa kwa watu binafsi kuwekeza na Halmashauri kupata asilimia kadhaa.

Aidha, waliipongeza timu ya menejimenti kwa kubuni miradi kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya mapato na kuishauri kujikita katika kusimamia miradi iliyopo ,ili fedha zinazozalishwa zitumike kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma na kuanzisha miradi mipya ya uwekezaji.

Mhe. Hanana Mfikwa, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako alisema kuwa,jambo la Halmashauri kujitegemea na kubuni miradi ni jambo la msingi na Halmashauri inahitaji kuanzisha vyanzo vya mapato , ambavyo vitasaidia kupunguza adha ya kufukuzana na wananchi kwenye kodi mbalimbali , hivyo ni vema vyanzo vilivyopo makusanyo yake yatumike kununua mzani au kuingia ubia na mzabuni au mwananchi anayeweza kuweka mzani kwa mfumo wa jenga,tumia rejesha na sio kubinafsisha.

Alisema kuwa, kubinafsisha kwa mtu binafsi kuweka mzani katika soko hilo haiwezekani ,kwani mwisho wa safari Halmashauri itakosa vyanzo vya mapato na kushindwa kubuni vyanzo vingine ,kwani vyanzo vyote vya mapato vitakuwa mikononi mwa wananchi na kuanza kukimbizana na wananchi kuhusu kodi.

Aliongeza kuwa,kwa sasa mambo yanayotakiwa kufanyika ni pamoja na uwekezaji wa Halmashauri, kwa Halmashauri kujipanga kuwekeza kupitia vyanzo vya mapato ambavyo imewekeza,hivyo kujenga kwa mfumo wa jenga,tumia,rejesha inawezekana vinginevyo Halmashauri ijenge mzani fedha zitakapo patikana.



**Hatuna katazo lolote la kutupa takataka kwenye dampo la Itengelo.**

**Na. Lina Sanga**

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Makambako, Mhe. Hanana Mfikwa katika mkutano wa baraza la Madiwani la robo ya kwanza katika mwaka wa fedha 2023/2024 uliofanyika novemba 7,2023 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri.

Mhe. Hanana alitoa kauli hiyo mara baada ya mjumbe wa baraza hilo kuhoji namna gani Halmashauri ya Mji Makambako imejipanga kupata eneo la kutupa taka, mara baada ya baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe kutoa tamko la kupinga matumizi ya dampo la Itengelo,lililopo Kata ya Saja kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Hanana alisema kuwa, Halmashauri haifanyii kazi vyombo vya habari bali vikao na Halmashauri ya Mji Makambako haina katazo

lolote la kutupa takataka kwenye dampo la Itengelo bali ruhusa ya kutupa taka kwenye eneo hilo na Halmashauri ya Wilaya ya Wang-ing'ombe ambao ndiyo wenye eneo wanajua na wana barua yenye ruhusa inayowataka kuipa Halmashauri ya Mji Makambako ush-irikiano kuhusu kutupa taka kwenye eneo hilo.

" Sisi kama Halmashauri hatuna katazo lolote la kutupa takataka kwenye eneo lile bali tuna ruhusa ya kutupa takataka kwenye eneo lile na linafaa kutupa takataka, na wao wenye eneo hilo wanajua na wana barua inayoturuhusu sisi na inayowataka wao kutupa ushirikia-no sisi kuhusu kutupa taka kwenye eneo lile kwa hiyo hii ndiyo taari-fa na ndiyo habari", alisema Mhe. Hanana.

Aidha, alisema kuwa wakati muafaka utakapofika wa kuwa na eneo mbadala kwa kadri ya mahitaji,zoezi la kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la kutupa taka linafany-iwa kazi na watendaji kama ambavyo maandalizi mengine yanavyofa-nyika kama ujenzi wa madarasa, nyumba,barabara na miundombinu mingine.





**Watumishi watakiwa kutunza na kuzithamini nyumba za Serikali wanazoishi kwa manufaa ya Umma.**

**Na. Lina Sanga**

Kamati ya fedha na uongozi ya Halmashauri ya Mji makambako imewataka watumishi kutunza nyumba wanazoishi ambazo zimejengwa na Serikali kwa kuzithamini kama za kwao na kufanya marekebisho madogo madogo inapobidi ili nyumba hizo zidumu muda mrefu.

Kamati ya fedha na Uongozi ilitoa rai hiyo novemba 2,mwaka huu katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa kipindi cha kuishia robo ya kwanza(Julai- Septemba) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 katika Kata ya Kitisi,Kitandililo na Mahongole.

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uongozi Mhe. Hanana Mfikwa akizungumza na watumishi wawili wa Zahanati ya Kijiji cha Ibatu,ambao wataishi katika nyumba mpya pacha iliyojengwa kupitia mfuko wa

kunusuru kaya masikini (TASAF) pamoja na wananchi, amewataka watumishi wote wanaokabidhiwa nyumba za Serikali kwa ajili ya kuishi kuhakikisha  wanazitunza kwaninyumba hizo ni zao hivyo hata kioo kikivunjika kununua kingine ni muhimu.



Pia,Mhe. Hanana  aliwapongeza wananchi wanaoshiriki katika usimamizi na utekelezaji wa  miradi katika maeneo yao kwa niaba ya Serikali,kwa kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati na kukamilika katika ubora unaoendana na thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali.

Lakini pia,aliwataka mafundi wakuu wanaotekeleza miradi ya Serikali kuhakikisha wanawalipa mafundi wanaowasaidia kazi kama vibarua kwa wakati ,ili kuepuka migogoro isiyokuwa na ulazima  na kuhakikisha wanakamilisha miradi ndani ya muda uliopangwa kwa viwango na ubora unaokubalika.

Alitoa rai kwa wananchi kuhakikisha watoto wote wanapata mahitaji muhimu kwa ajili ya ustawi wa watoto ikiwa ni pamoja na kupata chakula shuleni, na kuwataka wananchi wa Kijiji cha Usetule kujitoa kusafisha mazingira ya shule ya msingi shikizi  ya Magomati kwa kung'oa visiki ili iwe rahisi kwa Wakala wa barabara Mijini na Vijijini(TARURA) kutengeneza barabara za kudumu.

Kamati ya fedha na uongozi leo imefanya ziara na kukagua miradi minne

ambayo ni pamoja na kukagua miundombinu ya nyumba pacha ya Walimu shule ya sekondari Kitisi,ujenzi wa shule mpya ya sekondari Mbugani katika Kata ya Kitandililo,ujenzi wa nyumba pacha ya watumishi katika Zahanati ya Ibatu na Ujenzi wa madarasa sita na matundu 12 ya vyoo shule ya msingi shikizi Magomati.









## Hakuna kilichosimama Idofi –Mhe. Ummy Mwalimu

**Na. Lina Sanga**

Mhe Ummy Mwalimu,Waziri wa Afya amewahakikishia wakazi wa Mkoa wa Njombe kuwa hakuna kilichosimama katika ujenzi wa kiwanda cha mipira ya mikono cha MSD kilichopo Mtaa wa Idofi katika Halmashauri ya Mji Makambako.

Alitoa kauli hiyo oktoba 24,2023 katika ziara yake katika kiwanda hicho mara baada ya Mbunge wa jimbo la Makambako, Mhe. Deo Sanga kuhoji kuhusu ukamilishaji wa kiwanda hicho na aina ya bidhaa zitazozalishwa mbali na uzalishaji wa mipira ya mikono (gloves).

Mhe. Ummy alisema kuwa,chini ya Serikali ya awamu ya sita ya hakuna kilichosimama kwani ujenzi wa kiwanda hicho bado unaendelea na kwa mwaka huu kuna maendeleo makubwa ya mradi huo na Serikali kwa sasa imetoa Bil. 11 na itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi ya maende-

leo yote iliyoanzishwa katika Serikali ya awamu ya tano.
Pia,katika sekta ya Afya alisema kuwa ,wamedhamiria kuongeza uzalishaji wa ndani wa dawa,vifaa tiba na bidhaa nyingine za Afya ili kupunguza uhaba wa dawa na vifaa tiba, kwani kwa sasa bidhaa hizo asilimia 85 zinaagizwa nje kwa gharama kubwa na zinafika kwa kuchelewa nchini hivyo kusababisha uhaba wa dawa na vifaa tiba.

Aliongeza kuwa, lengo  la Serikali kujenga viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini ni kufikia  asilimia 50 ya bidhaa za Afya kununuliwa ndani ya nchi ifikapo 2030 kupitia Bohari kuu ya dawa (MSD) ambapo kwa  sasa ni asilimia 1



Aidha alisema kuwa,kwa sasa kuna jumla ya viwanda 30 vya dawa na vifaa tiba na viwanda 11 vinafanya kazi ikiwa ni pamoja na viwanda viwili vya uzalishaji chupa Mil. 90 za maji tiba (dripu) na mahitaji ni Mil 24 hadi 26 ,hivyo maji tiba hayatanunuliwa tena nje bali yataanza kununuliwa nchini.

Alibainisha kuwa,Bohari ya dawa (MSD) katika bajeti ya mwaka 2021/2022 imenunua bidhaa za Afya zilizotengenezwa ndani ya nchi zenye thamani ya Bil 14. 1,bajeti ya mwaka 2022/2023 imenunua bidhaa za Afya zenye thamani ya Bil. 39.4 matarajio kwa sasa ni kuhakikisha  ununuzi wa bidhaa hizo kufikia  Bil. 50 ifikapo kipindi cha kufunga mwaka wa fedha wa Bunge.

Alitoa rai kwa Mbunge wa jimbo la Makambako kuridhia kiwanda hicho kuanza na uzalishaji wa mipira ya mikono kwa sasa na mapendekezo ya Kamati iliyopita katika kiwanda hicho yatajadiliwa katika kikao cha pamoja cha kamati za Bunge za  uwekezaji mitaji ya Umma, Afya na masuala ya UKIM-



**Waziri wa Afya aridhia kondomu kutengenezwa kiwanda cha MSD Idofi.**

**Na. Lina Sanga**

Mhe. Ummy Mwalimu,Waziri wa Afya mnamo mwezi oktoba 24,mwaka huu aliridhia pendekezo la Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhe. Anthony Mtaka la kiwanda cha mipira ya mikono (MSD ) Idofi,katika Halmashauri ya Mji Makambako kuzalisha mipira ya kiume(Kondomu) kwani mali ghafi za uzalishaji zinaendana na mipira ya mikono inayozalishwa ki-



wandani hapo

Akiridhia pendekezo hilo,Mhe. Ummy alisema kuwa endapo bidhaa hiyo itazalishwa katika kiwanda hicho , itasaidia kupunguza gharama ya ununuzi wa bidhaa hiyo nje ya nchi ambapo kwa sasa jumla ya dola Mil. 10 zinatumika kununua kondomu.



Alisema kuwa,kwa sasa wanachotaka ni watu kuendelea kutumia kinga kwani UKIMWI na magonjwa ya zinaa bado yapo na kutokana na umuhimu wa bidhaa hiyo ni vema zitengenezwe ndani ya nchi na zitengenezwa katika kiwanda cha mipira ya mikono Idofi, katika Halmashauri ya Mji Makambako,Mkoani wa Njombe.



**Makamu wa Rais aweka jiwe la msingi kiwanda cha MSD Idofi na kuagiza ujenzi wa kiwanda hicho ukamilike na kianze kuzalisha ifikapo januari mosi,2024.**

**Na. Lina Sanga**

Makamu wa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Mhe. Dkt Philip Mpango ameuagiza uongozi wa Bohari ya Dawa nchini (MSD),kuhakikisha shughuli za uzalishaji katika kiwanda cha kutengeneza mipira ya mikono(gloves) kilichopo Mtaa wa Idofi,katika Halmashauri ya Mji Makambako unaanza kufanyika januari mosi,2024.

Dkt. Mpango alitoa agizo hilo oktoba 26,mwaka huu mara baada ya kuweka jiwe la msingi katika kiwanda hicho,na kuagiza uongozi wa kiwanda hicho pamoja na Wizara ya Afya kuandaa taarifa ya kina itayoeleza sababu ya kutofungwa kwa mitambo miaka miwili iliyopo kiwandani hapo pamoja na hoja za Mkaguzi mkuu wa Serikali (CAG).

Alisema kuwa changamoto za kiutendaji zilizopo katika kiwanda hicho zishughulikiwe na kuwahakikishia wakazi wa Idofi kuwa kiwanda hicho hakitahamishwa na kuzalisha dawa,vifaa tiba na vitendanishi.

Alimuagiza Naibu Waziri wa Wizara ya Afya na Naibu Waziri wa ofisi ya Rais TAMISEMI, kuhakikisha bidhaa zingine zizalishwe katika kiwanda hicho kwa kutumia miundombinu iliyopo kiwandani hapo kama maji tiba na vitendanishi vya maabara ili kuongeza tija.

Aidha,aliitaka kampuni tanzu ya MSD kuzingatia misingi ya kibiashara,ili waweze kujitegemea katika uzalishaji kutoka katika kiwanda cha Idofi na viwanda vingine na kuagiza uongozi wa kiwanda cha Idofi kuongeza ajira za wananchi wa idofi katika kiwanda hicho hasa wanawake.

Aliagiza Wakala wa barabara Mijini na Vijijini kufanya tathmini ya ya ujenzi wa barabara ya lami kuelekea eneo la kiwanda inayokadiriwa kugharimu shili Bil. 1.4 na kuifikisha ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya






TRA MIGOLI NA IRINGA WATAKIWA KUONDOA CHANGAMOTO YA KUPITISHA SHEHENA YA PARACHICHI ZA MWEKEZEZAJI AVOAFRICA.

Na. Lina Sanga

Makamu wa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Mhe. Dkt Philip Mpango ameitaka TRA Migoli na Iringa  kuhakikisha changamoto ya ucheleweshaji wa shehena za parachichi inaondolewa.

Mhe. Mpango alitoa agizo hilo oktoba 26,mwaka huu  mara baada  ya kupokea changamoto anazokabiliana nazo mwekezaji wa kiwanda cha usindikaji wa parachichi AVOAFRICA,kilichopo Mtaa wa Majengo, katika Halmashauri ya Mji Makambako ikiwa ni moja kati ya mradi alioutembelea katika ziara yake Mkoani Njombe.

Alisema kuwa, kitendo cha TRA Migoli na Iringa  kuzuia shehena ya parachichi kwa muda mrefu,inaweza kumsababishia mwekezaji hasara kubwa kwani zao hilo ni mali ya kuoza.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wote nchini katika maeneo yanayolimwa parachichi kutambua kilimo hicho ni fursa na kuwataka kuitumia fursa hiyo vizuri ,kwani soko la zao hilo ni kubwa na Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kwa sasa ndege ya mizigo imenunuliwa ili kuwezesha wawekezaji kusafirisha mizigo ikiwa ni pamoja na mizigo.




Pia,alisema kuwa changamoto ya uwanja wa ndege wa Njombe  ameisikia na kuahidi kuishughulikia chini ya Serikali ya Mama Samia kwani  ipo kazini na wanachotaka ni kuhakikisha maisha bora kwa watanzania na kila mmoja lazima awekeze jasho lake.

Alipongeza uwepo wa kiwanda cha AVOAFRICA ambacho uwekezaji wake umegharimu  dola za kimarekani takribani mil. 4.8 na kueleza kuwa kiwanda hicho ni cha mfano na kuwataka waandishi wa habari kueneza uwepo wa kiwanda hicho ili vijana wengi wavutiwe kuwekeza katika kilimo cha parachichi.

# MATUKIO KATIKA PICHA - MIRADI ILIYOTEMBELEWA NA KAMATI YA FEDHA ROBO YA KWANZA 2023/2024



**NYUMBA PACHA YA WATUMISHI WA ZAHANATI YA IBATU INAYOJENGWA KWA FEDHA ZA TASAF.**



**BAADHI YA MADARASA KATIKA SHULE YA MSINGI SHIKIZI MAGOMATI,KIJIJI CHA USETULE,KATA YA MAHONGOLE YALIYOJENGWA KWA FEDHA ZA TASAF.**

# MATUKIO KATIKA PICHA



**SHULE MPYA YA SEKONDARI YA MBUGANI ,KATA YA KITANDILILO INAYOJENGWA KWA FEDHA ZA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA UJIFUNZAJI (SEQUIP)**



**NYUMBA PACHA YA WALIMU,SHULE YA SEKONDARI YA KITISI INAYOJENGWA KWA FEDHA ZA TASAF.**

## NUKUU MBALIMBALI YA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI - BARAZA LA ROBO YA KWANZA



" Kiasi cha Mil. 104 kutumika kuanzisha mradi wa mzani ambao hatujawai fanya,na sera ya nchi yetu na Serikali inaema Serikali haitafanya biashara bali itajikita kukusanya kodi,nashauri mradi wa mzani ubinafsishwe kwa watu binafsi, alipe asilimia kadhaa kwa Halmashauri"

Mhe. Alimwimike Sawhi,diwani wa Kata ya Kivavi

# NUKUU MBALIMBALI YA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI - BARAZA LA ROBO YA KWANZA




"Nianze kwanza kwa kupongeza sana wakuu wa idara na kamati ya fedha kwa kuibua mradi wa Mil. 104 wa mzani katika soko la mazao kiumba na kuona unaweza kuwa na tija kwenye Halmashauri yetu , kwa sasa tuna miradi mitatu nashauri faida inayopatikana kwenye miradi hiyo itumike kuanzisha miradi mipya na sio kukopa"

Mhe. Salumu Mlumbe,diwani wa Kata ya Lyamkena

## MATUKIO KATIKA PICHA - ZIARA YA MAKAMU WA RAIS KIWANDA CHA MSD IDOFI NA AVOAFRICA















ISO 9001:2015 Certified
msd
II JIWE LA MSINGI LA
ANDA CHA

